**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MAGU**

***Unapojibu tafadhali taja:***

Kumb.Na.HA.38/293/01/4 Tarehe: 09 Februari, 2026

Wananchi Wote,
Wilaya ya Magu,
**MAGU - MWANZA.**

**YAH: TANGAZO LA NAFASI YA MWENYEKITI WA BODI YA AJIRA KWA HALMASHAURI YA WILAYA YA MAGU**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Magu kwa mujibu wa Kanuni ya 110 – 113 ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022 anapenda kuwatangazia watu wote wenye sifa kuomba kazi ya nafasi ya Mwenyekiti wa Bodi ya Ajira.

**MWENYEKITI WA BODI YA AJIRA – NAFASI MOJA (01)**

**A. SIFA ZA MWOMBAJI**

i. Awe raia wa Tanzania
ii. Awe Mkazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Magu
iii. Awe Mstaafu Serikalini
iv. Awe hajawai kushitakiwa kwa kosa lolote la Jinai
v. Awe na Umri kuanzia miaka 55 hadi 65 (Sitini na tano)
vi. Awe na Elimu ya Kidato cha nne au cha Sita
vii. Awe na Taaluma ya kuanzia Stashahada ya juu/Shahada katika fani ya Sayansi ya Jamii, Sheria, Utawala na Rasilimali watu.

**B. MAJUKUMU YA MWENYEKITI WA BODI YA AJIRA**

i. Kuongoza Vikao vya Bodi ya Ajira kwa mujibu wa Taratibu za Vikao
ii. Kuendesha/kuongoza vikao vya Usaili wa waombaji wa nafasi za kazi

### C. POSHO

i. Kazi hii haina mshahara wa kila mwezi, Mwenyekiti wa Bodi ya Ajira atakuwa analipwa posho kutokana na vikao vitakavyokaliwa na Bodi kwa mujibu mwongozo. Kwa kuzingatia Kanuni ya 113 ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022 Mwenyekiti wa Bodi ya Ajira atahudumu kuanzia tarehe ya kuteuliwa mpaka pale litakapovunjwa Baraza la Madiwani **(*Kipindi kisichozidi miaka mitano*).**

### D. MASHARTI YA JUMLA

i. Mwombaji aambatishe wasifu wake kwenye barua yake maombi
ii. Mwombaji aambatishe nakala ya vyeti vyake vya Elimu na Taaluma, kuzaliwa/kitambulisho cha Uraia (NIDA).
iii. Kila mwombaji aambatishe maombi yake na picha 2 za passport size
iv. Mwombaji asiwe kiongozi wa chama chochote cha siasa
v. Kila mwombaji aandike kwa usahihi, Anuani yake na namba ya simu inayopatikana muda wote.

Maombi yote yatumwe kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Magu kuanzia tarehe 10/02/2026 ya tangazo hili hadi tarehe 23/02/2026 saa 9.30 Alasiri

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya,
1078 Barabara ya Musoma,
334021078 Ilungu,
S.L.P 200,
**MAGU – MWANZA.**

Mohamed Ramadhani
**MKURUGENZI MTENDAJI**
**HALMASHAURI YA WILAYA**
**MAGU**

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
MAGU.